
# Zab. 33 - Onjeni muone

M: Jeannot Amani Mulume




**Shairi: 2-3, 10-11, 12-13, 14-15**

1. Nitamtukuza Bwana kila wa**kati**;
sifa yake kinywani mwangu sikuzo**te**.
Roho yangu ijisifu katika **Bwa**na:
wanyonge wasikia na **ku**furahi.

2. Mheshimuni Bwana enyi watakatifu **wake**,
kwa maana wenye kumheshimu hawakosi ki**tu**.
Watajiri wamegeuka maskini, wakaona **nja**a;
bali wanaomtafuta Bwana hawakosi **ki**tu chema.

3. Njooni, waana, mnisi**kie**:
nitawafundisha kumheshimu Bwa**na**.
Ni nani mtu anayependa u**zi**ma,
anayetaka siku za ku**o**na heri?

4. Zuilia ulimi wako u**baya**,
na midomo yako isiseme uwo**ngo**.
Uepuke na mabaya, utende **me**ma,
tafuta amani na ku**i**fuatia.

**Zaburi ya siku ya Mungu ya 20 katika mwaka B**

**Shairi: 2-3, 16-17, 20-21, 22-23**

1. Nitamtukuza Bwana kila wa**kati**;
sifa yake kinywani mwangu sikuzo**te**.
Roho yangu ijisifu katika **Bwa**na:
wanyonge wasikia na **ku**furahi.

2. Macho ya Bwana yawaangalia watenda **mema**,
na masikio yake yaelekea milio ya**o**.
Uso wa Bwana ni juu ya watenda ma**ba**ya,
ili angoe ukumbusho wao dunia.

3. Mateso ya mtu mwema ni **mengi**,
lakini Bwana amwopoa katika yo**te**.
Alinda mifupa yake **yo**te:
hata mmoja wake hau**ta**vunjika.

4. Ubaya unamwua mtu **mwovu**,
nao wenye kumchukia mtu mwema watapatili**zwa**.
Bwana anakomboa roho za watumishi **wa**ke,
wote waliomkimbilia hawatapati**li**zwa kamwe.

**Zaburi ya siku ya Mungu ya 21 katika mwaka B**

amanijeannot@gmail.com